**HALI YA CHOO NA BAFU**

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

UTANGULIZI

Hujambo na karibu tena katika kipindi cha sikiliza ujifunze juu ya afya. Leo utawasikia vijana watano wakiingia mashakani na mama mwenye nyumba wao. Yote yanatokea wakati mama mwenye nyumba anadai kodi yake. Lakini katika hali hiyo Simo, Hassan, Jimmy na Manuel wanajikuta wakigombana na mama huyo juu ya hali ya choo na bafu la bweni lao. Sikiliza mchezo huu ili ung'amue nini kitatokea. Utasikia vyoo vinamchango gani katika suala zima la afya na vipi unavyoweza kuepuka magonjwa. Tega sikio.

WAHUSIKA:
(Hassan, Simo, Steve, Jimmy, Manuel, Landlady)

KISA CHA KWANZA

SFX: Sauti za ndege, kuku mara moja moja, mama mwenye nyumba akitembea kwa kujiburuza akitumia mkongoja na akihema kwa tabu na vijana wakuzoa takataka wanasikika anatupa mawe mara nyingine, mbwa anamnusa nusa anampiga kwa fimbo,mbwa anambwekea..anajizungumzia.

MWENYE NYUMBA: (Kando ya Mic)
Nataka kuwategeshea wale vijana ili wanilipe pesa zangu. Ntawapata kabla hawajaamka niwaambie walale chini kifudifudi niwatie adabu kwa kuwacharaza matakoni kama vile wazazi wao wangefanya…Ni watoto wapumbavu sana. Miezi mitatu sasa hawajalipa kodi.

SFX: ANAGONGA MLANGO

MWENYE NYUMBA: Anha hawataki kuitikia.
Sasa ntatumia hii fimbo yangu..amkeni nyinyi..fungueni mlango, ni mama
Yenu mama mwenye nyumba.

SFX: SAUTI YA VITANDA VYA SPIRINGI

HASSAN: (kwenye mic akinong'oneza)
Jamaa amkeni..mwenye nyumba kaja.
Steve: (Akinong'oneza) Hassan usitusumbue bwana..
mwambie tumelala na ni kinyume na utamaduni wetu

kufungulia watu milango kabla hatujakunywa chai. Itatuletea kisirani.

SFX: MLANGO WABISHWA KWA NGUVU;JOGOO LAWIKA

MWENYE NYUMBA: Fungueni nyinyi watoto ni mama mwenye nyumba.

WOTE: (*Wapiga miayo na kujinyoosha vitandani*)

SIMO: (*Ananong'ona*) tuko mashakani. Manuel mambi bado tumelala. Anaweza kurudi baadae.

MANUEL:( *Kwa sauti ya chini*) Kwanini mimi Simo?

SIMO: (*Kwa sauti ya chini*) Mnaelewana.

SFX: (*Mlango unabishwa kwa nguvu*)

MWENYE NYUMBA: Fungueni la sivyo

MANUEL: (*Anapiga miayo huku akizungumza*). Oh mama
Bado tumelala.

MWENYE NYUMBA:
Upuuzi…Kwahiyo unaota unapozungumza na mimi sivyo Manuel?

STEVE: (*Akipiga miayo*) Si hivyo…tukusaidieje…unataka Chai.

MWENYE NYUMBA:
Msinichezee mimi. Nimekuja kuchukua kodi yangu ya nyumba.

JIMMY:(*Kwa sauti ndogo*) tufanye nini Manuel tuambie… We huyu mama ni rafiki yako.

MANUEL: (*Kwa sauti ndogo*) Tumwambieni tutalipa akitengeneza vyoo.

STEVE: Ok madam.. Hakuna tabu tutakulipa utakapotengeneza vyoo.

MWENYE NYUMBA:
Msiwe wapumbavu…Mna tabu gani nyie?

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

MANUEL: Wajua madam bafu tunayoogea haina sakafu. Kumewekwa mawe mawili tu sasa mtu inabidi awe na nguvu za kusimama vizuri kwenye mawe hayo ili apate kuoga vizuri.

MWENYE NYUMBA:
Niachieni upuuzi wenu huo…Ntaongeza mawe
Ikiwa ndo mnachotaka.

SFX: ANABISHA MLANGO KWA NGUVU

WOTE: WANAJIZUIA KICHEKO

SIMO: Madam…Twavaa nguo tutakufungulia subiri dakika moja tu…lakini kitu kimoja…

MWENYE NYUMBA: Mnasemaje?

SIMO: Chooo Madam

MWENYE NYUMBA: (*Anakosa subira*) Na je kuhusu choo?

SIMO: Ni mita tano tu kutoka mahala tunapolala na mara nyingine tunagombania nafasi na nzi waliojaa, choo chenyewe kinakuka vibaya sana, hawezi kulala, inaumiza sana

MWENYE NYUMBA: Hakuna la kufanya

SIMO: Na shida sio hiyo tu, choo hicho hakina dirisha. Mlango wake haufungiki na ukiwa kwenye haja kubwa huwezi kushughulika kwa makini manake wapigana na mlango tuuu.

STEVE: Na ukifanikiwa kuufunga mlango wenyewe, kuna vita vingine vinakungoja, kwa sababu si harufu hiyo inayokupata hadi unahisi kufa.

SIMO: Mtu hawezi kupumua uzuri… Mama… Choo chako bwana kinaua…Hakifai…Na ukweli wa mambo ni kuwa sikufungulii mlango ng'o.

MWENYE NYUMBA: (*Acheka kwa sauti*)
Hebu nambieni nyinyi watoto

Mlipokuwa mnakuja shule, wazazi wenu waliwaambia mshughulike na masomo au vyoo?

STEVE: Yote hayo …

MWENYE NYUMBA:
Nimesikia sauti ya Steve au nani? Sasa nyie wapumbavu… Ni lazima mufahamu kwamba mnajukumu la kufanya katika kutunza vyoo.

STEVE: Kwani sio wewe unaetakiwa kuviosha?

MWENYE NYUMBA:
Sawa kabisa na nyinyi mntakiwa muwe na jukumu Mnapovitumia kila mara mnapolewa mnakuwa hamna akili hata ya kuweza kutofautisha mdudu nani na nduvu nani. Mnakojoa ovyo mnakunya na kutapika mahala kokote na bila ya kujali chooni.

HASSAN: (*Anong'ona kwa sauti*) Ni simo na Steve.

STEVE: ShhhhhhhhShhhhh

MWENYE NYUMBA:
Kwa kweli hata hamna haja ya kuwa na vyoo.
Mtakuwa mkienda mwituni kufanya haja zenu… Yaani mnatazamia mimi niajiri mtu wa kuwaonyesha njia na namna ya kwenda haja kila mara mnapobanwa.

VIJANA: WACHEKA

MWENYE NYUMBA:
Mwajua nini, mkimanika na kutumia bongo zenu basi tunaweza kuelewana.

MANUEL: Maelewano aina gani?

MWENYE NYUMBA:
Angalieni.. Mkiwa mtasafisha choo chenu na bafu ntawapunguzia kodi ya nyumba.

HASSAN: Manuel, jamaa, dili safi hiyo…sasa hiyo itaamanisha tutalipa nusu ya kodi anayotudai.

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

MWENYE NYUMBA: Kwanini msifungue mlango tu tuzungumze.

SFX: MLANGO UNAFUNGULIWA:

MWENYE NYUMBA:
Harakisheni vijana, tokeni nje, tuelewane haraka
Msije mkachelewa kwenda shule.

SFX: SAUTI YA VITANDA NA MIGUU

MWENYE NYUMBA: Twendeni kule kwenye choo na bafu

## SURA YA PILI

SFX: WATU WAMENZA KUAMKA MAJUMBANI;MAJOGOOO HUKU BAISKELI ZAPITA:

MWENYE NYUMBA:
Angalieni vijana, mpango wenyewe ni huu. Nyie Mtasafisha choo hiki na bafu halafu ntawapunguzia kodi. Mwasemaje?

WOTE: (*wote wakubaliana kwa njia tofauti wengine wasema sema wengine waitikia*)

STEVE: Mama tumekubaliana,lakini kusema kweli vyoo vyako hivi viko katika hali mbaya sana sijui hata mtu ataanzia wapi.?

MWENYE NYUMBA:
Kijana mzuri Steve… Unaweza kutumia sabuni na maji, chukua mti mrefu ufunge na tambara bovu bovu tumbukiza kwenye maji ya sabuni halafu pangusa chini basi kazi imekwisha. Likaushe tambara lako juani ili utumie siku nyingine na mufagie kila siku.

JIMMY: Lakini madam na kuhusu harufu? Choo chanuka kweli.

MWENYE NYUMBA:
Ni rahisi, tafuteni nyasi za kukauka zitumieni kufunikia choo halafu mzichome nyasi hizo zikitumbikia ndani ya choo zitaleta harufu nzuri.

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

WOTE: (*Hawana mbavu kucheka*)

SIMO: Sasa tunazungumzia kuhusu malipo nusu au kodi yote ya nyumba ikiwa tutakubaliana mpango huu.

MWENYE NYUMBA:
Simo shida yako ya pesa haiishi wewe… kwa deni ninawadai mtaondoa asilimia 20 na mwezi ujao mtaondoa asilimia 30 mnilipe zilizosalia.

MANUEL: Sawa madam nafikiri ni dili poa.

MWENYE NYUMBA: (*Anaondoka*)
Ikiwa hamtaniletea pesa zangu ntazifuata… mnajua tunaweza kufanya hivi. Haina haja ya kukaa na vyoo vyakunuka ni lazima kuwe mahala mnakoweza kukaa chini na kunywa chai na kusoma vitabu vyenu.

WOTE: WACHEKA

MWISHO MUZIKI

WAZUNGUMZAJI WAWILI:

**Je Wajua?**

Ni nusu tu ya Afrika iiliyo na uwezo wa kupata maji na huduma za vyoo na mitaro. Huduma hii ina maana ni utoaji na ufikishaji wa njia za kutupa kinyesi kwa hali iliyo salama kwa afya. Hii ni muhimu kwa ajili ya kuwaepusha watu wasipate maradhi.